# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA WAZIRI MKUU

**Anuani ya Simu: "TAMISEMI"**
**Simu Na**: (026) 2322848, 2321607
2322853, 2322420
Nukushi: (026) 2322116, 2322146
2321013
**Barua pepe:** *ps@pmoralg.go.tz*

**Tawala za Mikoa na**
**Serikali za Mitaa,**
**S.L.P. 1923,**
**DODOMA.**

***Unapojibu tafadhali taja:***
***Kumb.*** Na.**CCE.3/215/01/79**

**09 Julai, 2015**

Makatibu Tawala wa Mikoa,
**TANZANIA BARA.**

**Yah: MWONGOZO WA UANZISHAJI NA MATUMIZI YA AKAUNTI MPYA TATU (3) ZA BENKI ZA SEKTA YA MAJI, SEKTA YA ELIMU NA SEKTA YA AFYA NA KUFANYA KILA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA KUWA NA JUMLA YA AKAUNTI ZA BENKI TISA (9)**

Tafadhali, husikeni na somo lililotajwa hapo juu.

Mtakumbuka kuwa mwaka 2012, Serikali ilifanya maamuzi ya kupunguza akaunti za Benki kutoka wastani wa benki akaunti 60 kwa kila Halmashauri mpaka akaunti 6. Zoezi la upunguzaji wa akaunti za benki lilikwenda sambamba na usimikaji wa mfumo wa IFMS-Epicor 9.05 katika Halmashauri zote.

Matumizi ya akaunti 6 sambamba na mfumo wa Epicor 9.05 ulianza rasmi Julai, 2012 kwa Halmashauri 133. Zoezi hilo limeendelea kwa mafanikio na kuleta tija katika usimamizi wa fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Pamoja na Serikali kufanya maamuzi ya kupunguza Akaunti za Benki kama nilivyoeleza hapo juu, bado kumekuwa na uhitaji wa akaunti za benki kwa miradi na Sekta zinazotekeleza mikakati ya

Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa (*Big Results Now*, BRN) kwa lengo la kuongeza uwazi na ufanisi katika usimamizi wa fedha zinazotumika kwenye sekta hizo.

Kutokana na hali hiyo, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI imeridhia kuongeza akaunti 3 zifuatazo kuanzia mwezi Julai, 2015:-

(a) Akaunti ya Maji
(b) Akaunti ya Elimu na
(c) Akaunti ya Afya

Kati ya akaunti hizo, Akaunti ya maji tayari ilishafunguliwa na imeendelea kutumika mintaarafu barua yangu yenye Kumb. CCA.3/151/01/27 ya tarehe 20/5/2013. Hata hivyo, Mwongozo unaotumika sasa ulikuwa haujahuishwa ili kujumuisha akaunti hiyo.

Hivyo basi, ili kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza uamuzi huu, OWM-TAMISEMI imeandaa Mwongozo wa uendeshaji wa akaunti 3 nilizozitaja hapo juu kwa lengo la kuanza kutekelezwa kwa Hesabu za mwaka wa fedha 2015/2016.

Hivyo, kwa barua hii, wajulisheni Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizoko katika Mikoa yenu kuhakikisha wanazingatia mambo yote yaliyoainishwa kwenye Mwongozo ulioambatanishwa na barua hii.

Nawatakia utekelezaji mwema.

J.A. Sagini
**KATIBU MKUU**

**Nakala:** Katibu Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu,
2 Mtaa wa Magogoni,
S.L.P 3021,
**11410 DAR ES SALAAM.**

Katibu Mkuu,
Wizara ya Fedha,
1 Barabara ya Madaraka
S.L.P 9111,
**11468 DAR ES SALAAM.**

Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi,
7 Mtaa wa Magogoni,
S.L.P 9121,
**11479 DAR ES SALAAM.**

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maji,
426 Barabara ya Morogoro,
S.L.P 9153,
14473 DAR ES SALAAM.

Katibu Mkuu,
Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii,
6 Barabara ya Samora Machel,
S.L.P 9083,
**11478 DAR ES SALAAM.**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
S.L.P 9080,
**DAR ES SALAAM.**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MWONGOZO WA MATUMIZI YA AKAUNTI 3 ZA BENKI ZA MRADI WA MAJI, SEKTA YA ELIMU NA AFYA KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

30 JUNI, 2015


*Imetolewa na:*

**OWM-TAMISEMI**

**S.L.P 1923**

**DODOMA.**

***Simu Na:*** *(026) 2322848, 2321607*
*Nukushi: (026) 2322116, 2322146*
***Barua pepe:*** ps@pmoralg.go.tz


**JUNI, 2015**

## MWONGOZO WA MATUMIZI YA AKAUNTI 3 ZA BENKI ZA MRADI WA MAJI, SEKTA YA ELIMU NA AFYA KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

**Utangulizi:**

Mwongozo huu umeandaliwa ili kurahisisha uratibu na utekelezaji wa maamuzi ya Serikali ya kuongezeka kwa idadi ya Akaunti za Benki za Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka Akaunti sita za Benki hadi kufikia Akaunti tisa.

Nyongeza ya Akaunti za Benki ni hatua ya kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika maeneo ya Afya na Elimu. Hatua hii inatokana na hatua tuliyoifikia katika matumizi ya Mfumo wa Epicor na Mazingira yaliyopo sasa. Ni dhamira ya Serikali kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji, hivyo kila itakapotokea fursa na changamoto hatua stahiki zitachukuliwa ili kukabili hali hiyo. Maandalizi ya Mwongozo huu yamezingatia Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 na Kanuni za Usimamizi wa Fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa "*Local Authorities Financial Memorandum*" (LAFM), 2009. Mwongozo huu ni nyongeza ya mwongozo wa Akaunti sita wa tarehe 30 April 2012

Akaunti mbili mpya za Benki zilizoongezeka za sekta ya Elimu na Afya zitakazofunguliwa zitaanza kutumika kuanzia tarehe 1, Julai,

2015, Akaunti ya Sekta ya Maji itaendelea kutumika kama ilivyokuwa hapo awali (isifunguliwe mpya). Hii ina maana kuwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kutakuwa na Jumla ya Akaunti za Benki tisa (9) kama zilivyo orodheshwa hapa chini:

*(i)* Akaunti ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri (*Council Own Source Collection Account)*

(ii) Akaunti ya Mishahara (*Personnal Emmoluments Account*)

*(iii)* Akaunti ya Matumizi ya Kawaida (*Other Charges Expenditure Account)*

(iv) Akaunti ya Maendeleo (*Development Account)*

(v) Akaunti ya Amana Mbalimbali (*Miscellaneous Deposits Account)* na

(vi) Akaunti ya Mfuko wa Barabara (*Road Fund Account*).

(Vii) Akaunti ya mradi wa Maji (*Water Sector Account*)

(Viii) Akaunti ya sekta ya Elimu (*Education Sector Account*)

(ix) Akaunti ya sekta ya Afya (*Health Sector Account)*

Mwongozo huu una sehemu kuu mbili; Sehemu ya kwanza inahusu maelekezo ya namna ya kuhamisha fedha toka akaunti za Matumizi mengineyo (OC) na Akaunti ya Maendeleo (Development) kwenda kwenye akaunti mpya zitakazofunguliwa, sehemu ya pili inahusu

maelekezo ya namna ya uendeshaji wa mfumo mpya wa akaunti tisa kwa kutumia mfumo wa IFMS (Epicor 9.05)

.

## SEHEMU YA KWANZA

## MAELEKEZO YA NAMNA YA KUHAMISHA FEDHA KUTOKA KATIKA AKAUNTI ZA MATUMIZI MENGINEYO (OC) NA MAENDELEO ( DEVELOPMENT) KWENDA KWENYE AKAUNTI MPYA ZITAKAZOFUNGULIWA

Akaunti zinazofunguliwa zitajulikana kama akaunti za Ki-sekta hii ina maana kwamba fedha zote za matumizi ya kawaida yaani *Recurrent* zitaingizwa katika akaunti hizi.

A. **Akaunti ya Sekta ya Elimu** itatumika kupokea na kulipa fedha zote za Elimu ikiwa ni Elimu ya Msingi ,na Elimu Sekondari pamoja na Elimu ya watu wazima *yaani Formal and Non Formal Adult Education.* Ndani ya akaunti hii zitalipwa fedha kutoka vyanzo vyote kwa fedha za aina tajwa hapo juu pamoja na zitakazojitokeza ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida. Hivyo fedha za ndani zilizo kasimiwa kwenye elimu zitahamishwa kutoka Akaunti ya Mapato ya Ndani kwa utaratibu wa kawaida wa *"fund transfer"* na kutumika kupitia Akaunti hii ya Sekta ya Elimu.

B. Akaunti ya Sekta ya Afya itatumika kupokea na kulipa fedha zote ambazo ni za matumizi ya kawaida *Recurrent nature*. Hivyo akaunti hii itatumika kulipa fedha za ruzuku kutoka Serikali kuu, fedha za Basketi kutoka mfuko wa pamoja wa wahisani, fedha za ndani kutoka vyanzo vya Halmashauri pamoja na fedha za aina hiyo zitakazojitokeza.

1. Zoezi la kuhamisha fedha za Elimu na Afya kwenda Akaunti mpya litafanyika baada ya kukamilisha usuluhishi wa Benki. Bakaa za akaunti zote zitawasilishwa OWM - TAMISEMI Dodoma kwa ajili ya kuingizwa kwenye Mfumo wa IFMIS Epicor 9.05.

2. Halmashauri zinatakiwa kuwasilisha taarifa za usuluhishi wa hesabu (Benki Reconciliation) za Akaunti zote kwa kipindi kinachoanzia 1 Julai, 2014 hadi 30Juni, 2015, kabla au ifikapo tarehe 15 Julai 2015. Taarifa hizo za usuluhishi ziwasilishwe pamoja na viambatanisho vyote na mchanganuo unaoonyesha bakaa kwa kila Akaunti na chanzo cha fedha husika kwa kipindi cha Julai 2014 hadi June 2015.

3. Kila Halmashauri inatakiwa kuhamisha fedha zote zitakazo oneshwa kama bakaa kwa Idara za sekta ya Elimu na Afya baada ya tarehe 1,Julai 2015 na kabla ya tarehe 31 Julai 2015

## SEHEMU YA PILI

## MAELEKEZO YA UENDESHAJI WA AKAUNTI TISA ZA BENKI KATIKA MFUMO WA IFMS - EPICOR 9.05.

1. Mfumo wa Epicor 9.05 umeandaliwa kwa kuzingatia mabadiliko ya kuongeza idadi ya akaunti za Halmashauri hadi kufikia akaunti tisa kwa kila Halmashauri. Kila Mradi au Chanzo cha fedha kimepewa alama (codes) ambayo itasaidia ufuatiliaji wa mapato na matumizi kwa vyanzo vya fedha na miradi.

2. Kupitia mfumo wa Epicor 9.05, Kila Mkuu wa Idara au Kitengo mwenye fedha katika bajeti ya Halmashauri anatakiwa kuzingatia taratibu za fedha kama zilivyoelekezwa kwenye LAFM, 2009. Hii ni pamoja na kuhakikisha mgawo wa fedha (*fund allocation)* unafanyika na matumizi ya fedha yanaelekezwa

katika vifungu sahihi kwa kuzingatia chanzo cha fedha, shughuli husika na aina ya matumizi yaani *GFS*.

Wakuu wa Idara za Afya, Elimu na Maji, kama Wakuu wa Idara na vitengo vingine watatakiwa kuwajibika kutoa idhini ya malipo yote kwa kuanzisha malipo au kupitisha malipo kwenye hati ya malipo kama Mwanzishaji (*initiator)* wa malipo kwa fedha za idara yake au kitengo ili matumizi ya fedha zinazohusu Idara/Kitengo chake zifanyike. Mkuu wa Idara anayo haki ya kupata taarifa ya mapokezi na matumizi ya fedha katika maeneo yanayohusu Idara/ Kitengo kwenye Mfumo wa IFMS. Utaratibu wenye usalama na rahisi uandaliwe na kila Halmashauri ili kuwawezesha Wakuu wa Idara zote kutumia fursa hiyo kwa ajili ya kutekeleza wajibu wao wa kusimamia matumizi ya Idara zao. Utaratibu huo uwasilishwe kwa Katibu Tawala wa Mkoa baada ya kuidhinishwa na Kamati ya Fedha na Uongozi ya Halmashauri ifikapo Julai 15, 2015.

3. Maelekezo ya Mpangilio na Uendeshaji wa Mfumo wa Malipo kwa kutumia mfumo wa IFMS- Epicor 9.05 unazingatia maagizo yaliyomo katika Kanuni na Taratibu za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa, (Local Authorities Financial Memorundum, 2009). Kwa kuwa matumizi ya Mfumo huu katika uingizaji data

na utoaji taarifa unahusu watu wachache watakao idhinishwa kwa sasa; Mweka Hazina (kwa kuzingatia na bila ya kupotosha maana na maelekezo yaliyopo katika aya ya pili hapo juu) atatakiwa kuandaa taarifa kila mwezi kwa kila Mkuu wa Idara mwenye fedha kwenye akaunti za Halmashauri ikionyesha mtiririko wa mapokezi na matumizi ya fedha za kila chanzo. Maelekezo haya yapelekwe kwenye Kamati ya Fedha na Uongozi ikiwa ni Mwongozo mahsusi wa utayarishaji wa taarifa ambayo ni sehemu ya utaratibu wa udhibiti wa ndani kwa mujibu wa agizo Na. 11 la Kanuni na Taratibu za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa, (Local Authorities Financial Memorandum, 2009).

4. Hati za malipo zitawekwa saini na Mkuu wa Idara za Afya, Elimu na Maji/ au Mtumishi aliyeidhinishwa na Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango. Mkurugenzi ataidhinisha Malipo au mtu yeyote atakayeteuliwa na Mkurugenzi na kuidhinishwa na Kamati ya Fedha na Uongozi.

   Hati ya Malipo (PV) itakuwa na saini za watumishi watatu ambao ni:-

   (i) Mhasibu aliyeandaa hati ya malipo.
   (ii) Mkuu wa Idara kwa fedha husika.

(iii) Mkurugenzi (Authorising officer) au mtu yeyote atakayeteuliwa na Mkurugenzi na kuidhinishwa na Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.

5. Kwa kuzingatia matakwa ya LAFM, 2009, Waweka sahihi (*Signatories*) watatu katika hundi za Akaunti za Benki kwa kila kundi watateuliwa na Mkurugenzi na kuidhinishwa na Kamati ya Fedha na Uongozi kama ifuatavyo:

Kundi B

i. Mkurugenzi

ii. Mweka Hazina

Kundi A

i. Mkuu wa Idara husika

ii. Msaidizi wa mkuu wa idara au mratibu wa Mradi

Kwa akaunti ya Sekta ya Elimu

i. Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi

ii. Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari

Maelekezo zaidi ya uwekaji wa hundi ni kama ilivyoelekezwa kwenye mwongozo wa akaunti sita wa April 2012. Aidha, waweka saini wote watateuliwa na Mkurugenzi na

Wataidhinishwa na Kamati ya Fedha na Uongozi kabla ya kuanza kutekeleza wajibu wao huo.

## HITIMISHO

Mara baada ya kupokea Mwongozo huu kila Mkurugenzi wa Halmashauri anaagizwa auwasilishe kwenye vikao halali vya Halmashauri kwa ajili ya kutolewa maamuzi ya utekelezaji.

J.A. Sagini
**KATIBU MKUU**
***Ofisi ya Waziri Mkuu***
***Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa***
***Julai 09, 2015***